JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI MIYOMBONI
S.L.P.1427,
IRINGA.
+255754676265
01/12/2020

Kumb. Na. MIYSS/UTA/Vol.1/....

Jina la Mwanafunzi.....

.....

S.L.P. .....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MIYOMBONI ILIYOPO MANISPAA YA IRINGA MWAKA 2020

1.0 Utangulizi

Ninayofuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka 2021. Shule ya sekondari Miyomboni ipo umbali wa km 1 kutoka stendi KUU YA DALADALA, nyuma ya Kituo cha Magereza na Hospitali ya Rufaa Iringa.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021.

Wanafunzi wanaoanza kidato cha kwanza (1) wataanza kupokelewa tarehe 11/01/2021, mwisho wa kupokelewa ni tarehe 31/01/2021 na mtoto atatakiwa afike siku hiyo pamoja na vitu vifuatavyo;

a. Fomu ya kukubali nafasi
b. Fomu iliyojazwa na Daktari kuthibitisha afya ya mwanafunzi (Hospitali ya Aserikali)
c. Picha mbili za mwanafunzi na moja ya mzazi/mlezi
d. Faili (spring file)
e. Bunda 1 la karatasi 500 (rimu) ya A4 anaporipoti
f. Fagio 2 za chelewa kwa wote (Wasichana na Wavulana)
g. Wasichana wote waje na jembe moja na fyekeo (kwanja)
h. Wavulana wote waje na leki moja na fagio ngumu (hard blooms)

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za shule

Wasichana

a. Sketi mbili za rangi ya kijivu (kitambaa kilichoambatanishwa kwenye fomu hii) zenye rinda box zinazofika karibu na unyayo wa miguu
b. Mashati mawili meupe yenye mikono mirefu.

c. Sweta la bluu yenye shingo ya V.
d. Fulana (T – shirt) yenye nembo ya shule;
e. Jozi mbili za viatu vya ngozi vyeusi vya kamba na visiwe na kisigino kirefu;
f. Soksi nyeupe jozi mbili.
g. Tai ndefu rangi ya kijivu

Wavulana

a. Suruali mbili za rangi ya kijivu zenye marinda mawili na mkunjo chini (turn up);ambazo hazijabanwa chini
b. Mashati mawili meupe mikono mirefu
c. Fulana (T – shirt) yenye nembo ya shule;
d. Sweta la bluu yenye shingo ya V;
e. Jozi mbili za viatu vya ngozi vyeusi vya kamba na visiwe na kisigino kirefu;
f. Soksi nyeupe jozi mbili;
g. Mkanda wa suruali mweusi usiwe wa utambi wala nembo yoyote.
h. Tai ndefu rangi ya kijivu

Tafadhali zingatia mavazi ya heshima yasiyobana kwa wavulana na wasichana.

Vazi la wanafunzi waislamu wa kike

a. Hijabu nyeupe ndefu, inayofika kiganjani ukinyosha mikono (mitandio haikubaliki)
b. Mashati mawili meupe mikono mirefu
c. Sketi mbili za rangi ya kijivu (kitambaa kilichoambatanishwa kwenye fomu hii) zenye rinda box zinazofika karibu na unyayo wa miguu

3.0 MAVAZI YA MICHEZO

3.1 Michezo inafanyika shuleni, mwanafunzi anatakiwa kuja na traki suti ya kijivu pana yenye mistari myeupe iliyoshuka chini (kitambaa cha kuteleza) itakayo valiwa siku rasmi itakayotangazwa kwa ajili ya michezo

4.0 Mahitaji muhimu ya mwanafunzi.

- Daftari kubwa 14 (counter book), dictionary mbili (Kiingereza-Kiingereza)
- Rula, penseli na mkebe (mathematical set).
- Begi la kubebea vitabu (Mifuko ya Rambo hairuhusiwi)

5.0 Sheria na kanuni za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
d) Kufahamu mipaka ya shule na kufahamu kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wa uanafunzi wako katika shule hii;
e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
g) Kuzingatia ratiba ya shulle wakati wote
h) Kutunza mali za umma.
i) Mwanafunzi **asipofika shule bila taarifa, mzazi atalazimika kufika shule na kutoa maelezo**
j) Mwanafunzi hataruhusiwa kutoka mazingira ya shule bila kibali maalumu
k) Lugha inayotumika shuleni ni **kiingereza tu.**
l) Mwanafunzi haruhusiwi kuingia sehemu za starehe kama vile nyumba za wageni, baa, music library
m) Mwanafunzi haruhusiwi kuingia ofisini bila ya kibali/ruhusa ya mwalimu.

6.0 **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:**

a) Wizi
b) Uasherati, usagaji na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupiga au kupigana.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito /kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi.
n) Utoro/kutokufika shuleni

7.0 **Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi:**

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara tu utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo bianafsi ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

8.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo na kuyatekeleza kikamilifu.

.....

MKUU WA SHULE

MEDICAL EXAMINATION FORM

MIYOMBONI SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 1427,
IRINGA

To be completed by medical officer in respect of all form entrants

Full name .....
Age .....
Blood count (Red and White).....
Stool examination.....
Urine analysis .....
Syphilis test .....
Eye test .....
T.B. test .....
Ear test .....
Chest test .....
Spleen .....
Abdomen .....

ADDITIONAL INFORMATION: e.g Physical or chronically of family disease etc.
.....
.....
.....

I certify that tha above student is fit to pursue secondary studies
Signature .....
Designation.....
Section .....

Date .....

Note
PUPIL: You must bring this form to school. No pupil may be enrolled without certificate of physical fitness.

.....
NDIJUYE, M.L
MKUU WA SHULE

JAMHURI YA MUUNGANO W TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI MIYOMBONI

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YAKE

A. UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI

Mimi ..... nimesoma kwa makini barua ya maagizo ya kujiunga na shule na sheria za shule. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa nakubali/ninaikataa nafasi hiyo kwa sababu ..... pia nayakubali/ninayakataa masharti/sheria za shule.

B. UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Mimi ..... mzazi/mlezi wa ..... ambaye amechaguliwa kujiunga na shule hii nimesoma maagizo ya shule na sheria zake. Ninakubali nafasi hiyo (kwa anayekubali). Ninaahidi kumtimizia mtoto wangu maagizo yote ya kujiunga na shule kwa muda uliopangwa. Pia nitashirikiana daima na uongozi wa shule katika kukuza na kumlea mtoto wangu.

Ahsante.

Jina la Mzazi/mlezi .....
Anwani .....
Kata/Mtaa ninaoishi .....
Simu ya nyumbani/kazini .....
Tarehe ..... sahihi .....

- Futa lisilohusika
- Mzazi/Mlezi akibadilisha anwani au kuhama atujulishe mara moja anwani mpya na makazi mapya

NB
Iwapo mwanao ana tatizo la kihistoria kama kifafa, na mengineyo, tujulishe.

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI MIYOMBONI

FOMU YA KUPOKELEWA SHULENI

1. Jina kamili .....
2. Mahali alipozaliwa .....
3. Utaifa .....
4. Tarehe ya kuzaliwa .....
5. Anwani ya nyumbani .....
6. Anwani ya mzazi/mlezi (kama tofauti na hapo juu) .....
7. Jina la mzazi/Mlezi .....
8. Ndugu wa karibu: -

NA	JINA	UHUSIANO	MTAA	SIMU
1				
2				
3				
4				

9. Dini .....Dhehebu.....
   Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini au dhehebu bila idhini mzazi/mlezi.
10. Kidato alichopokelewa .....
11. Shule aliyotoka mwanafunzi .....Wilaya.....Mkoa.....
12. Shughuli unazopendelea mbali na masomo kama mpira wa miguu, wa mikono, riadha, kuimba n.k.....

Sahihi ya mwanafunzi .....Tarehe.....
Sahihi ya Mzazi/Mlezi .....Tarehe .....